# NOTI MPYA KUANZA KUTUMIKA FEBRUARI MOSI

mjasiriamali @mjasiriamali @mjasiriamali


# MJASIRIAMALI

KAMATA FURSA

Tovuti www.mjasriamari.co.tz/ ISSN 3456-1679. NA. 08, Alhamisi Januari 23, 2025 Bei Tsh. 1,000/= Ksh 100


**WAONE NA WASIKIE...**

# DK. SAMIA AUPIGA MWINGI UWEKEZAJI

"TIC sasa hivi tuna kituo cha 'One Stop Center' ambapo ukifika pale unaweza ukasajili na ukaanza shughuli zako ndani ya siku tatu. "Tunaendelea kuhamasisha Watanzania waje TIC kusajili na kuwekeza kwani kuna faida wazawa wanapata, ikiwa ni pamoja...



- ASAJILI MIRADI 901 YA UWEKEZAJI KWA MWAKA 2024 YENYE THAMANI YA DOLA BILIONI 9.3
- IMEPIKU MIRADI 500 ILIYOSAJILIWA MWAKA 2023 ILIYOKUWA NA THAMANI YA DOLA BILIONI. 5
- HII NI SAWA NA ONGEZEKO LA ASILIMIA 44.5

# UZALISHAJI CHAI KUONGEZEKA 2030



# WAMACHINGA WATU SAHIHI KATIKA NCHI ILIYO SAHIHI



# CHUMA ULETE INAVYOWAKONDESHA WENGI

- ENDELEA KUSOMA HABARI HII KWA KINA

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wachuuzi na wafanyabiashara... UK.2

# DK. SAMIA AUPIGA MWINGI UWEKEZAJI

NA MWANDISHI WETU

TANZANIA imezidi kupaa katika uwekezaji, huku ikielezwa yote hayo yanatokana na jitihada za dhati zinazofanywa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuvutia wawekezaji wa ndani nan je ya nchi.

Katika kudhihirsiha Dk. Samia hana utani katika hilo ni kutokana na idadi kubwa ya wawekezaji wanaojitokeza nchini kila mwaka, hivyo kufanya rekodi zake kuendelee kupaa mwaka hadi mwaka.

Hii inathibitishwa na miradi 500 ya uwekezaji iliyosajiliwa mwaka 2023 wakati ndani ya mwaka 2024 imesajiliwa miradi ipatayo 901.

Kubwa zaidi wakati miradi 500 ya mwaka 2023 ilikuwa na thamani ya dola za kimarekani bilioni tano, miradi 901 iliyosajiliwa mwaka 2024 ina thamani ya dola za kimarekani bilioni 9.3.

Hayo yamethibitsihwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo Cha Uwekezaji Nchini (TIC), Dk. Binileth Mahenge aliyesema mwamka wa usajili wa miradi ya uwekezaji umeongezeka kutokana na fursa zinazotolewa na Rais Dk. Samia.

Akiwa mkoani Geita, Dk. Mahenge amekiri mafanikio hayo yametokana na uboreshaji wa mazingira bora ya uwekezaji pamoja na na mabadiliko ya uwekezaji mwaka 2022 ambayo imeondoa vikwazo vingi kwenye usajili wa uwekezaji.

"TIC sasa hivi tuna kituo cha 'One Stop Center' ambapo ukifika pale unaweza ukasajili na ukaanza shughuli zako ndani ya siku tatu.

"Tunaendelea kuhamasisha Watanzania waje TIC kusajili na kuwekeza kwani kuna faida wazawa wanapata, ikiwa ni pamoja na kuondolewa baadhi ya vikwazo.

"Hapa Geita mwaka jana walisajili miradi 18 na malengo ya mwaka huu ni kusajili miradi 50 kwa sababu mazingira ni rafiki," alisema Dk. Mahenge.

Mmoja wa wafaidika wa mazingira mazuri ya uwekezaji yaliyowekwa na Dk. Samia ambaye ni Rais wa Kampuni ya Mwamba Mining iliyopo Geita, Eduard Cornew ameeleza kuguswa na sera rafiki katika sekta ya madini hususani kwa wazawa na wabia wanaokuja kuwekeza na kuahidi kupanua uwigo wa uwekezaji.

Mkurugenzi Mtendaji (CEO) wa Kampuni ya Mwamba Mining, Thomas Cornew kutoka nchini Marekenai amrkiri kuwa tangu wamefika Tanzania wamepata ushirikiano mkubwa na hawajapata kikwazo kuwekeza.

Meneja wa Kampuni ya Mwamba Mining, Calvin Habil amesema mradi huo una thamani ya bilioni 8.5 umetumia miezi sita tangu kuanza hadi kufikia hatua ya majaribio kutokana na mazingira mazuri ya TIC.

"Ujenzi wa Mradi ulianza mwezi Mei, 2024 mapaka sasa tupo kwenye kipindi cha majaribio, kuweza kuona ufanisi wa kazi yetu tuna mpango wa kutanua plant yetu tuweze kuchakata tani 500 kwa siku."

Tayari Serikali imeendelea kuita wawekezaji na kusema, ujio wao unasaidia kwa kiwango kikubwa kutoa ajira na kukuza pato la Taifa.

# UZALISHAJI CHAI KUONGEZEKA 2030

NA MWANDISHI WETU

UZALISHAJI wa chai chakavu unatarajiwa kuongezeka hadi kufikia tani 30,000 za chai chakavu iliyosindikwa ifikapo mwaka 2030, lengo kubwa ikiwa ni kuwainua kiuchumi wakulima wadogo wa zao hilo.

Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania (TSHTDA) ndiyo iliyojipanga ifikapo mwaka 2030 kuzalisha tani 30,000 za chai kavu iliyosindikwa.

Hii ndiyo mikakati iliyowekwa kwenye uzalishaji wa zao hilo ili mkulima mdogo wa chai nchini aweze kupiga hatua kwenye kilimo hicho.

Kwa sasa wakulima hao wanazalisha tani 13,000 ambazo hazijitoshelezi, hivyo moja ya mkakati waliyojiwekea kama wakala ni kuhakikisha uzalishaji unaongezeka.

Miongoni mwa mikakati yao ni kujipanga kuhakikisha wakulima wanafikia uzalishaji tani 30,000 za chai kavu iliyosindikwa, naamini itafikia hivyo kutokana na serikali kutoa mbolea ya ruzuku.

TSHTDA inafahamu moja ya changamoto inayowakabili wakulima ni uuzaji wa chai kwa bei ndogo, jambo linalosababisha kushindwa kumudu kulima kwa wingi zao hilo.

Kutokana na hilo, TSHTDA imeingia mkataba na kampuni kadhaa kwa ajili ya kutoa huduma za ugani wakati wowote kwa wakulima katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Pia wakulima walitakiwa kuchangamkia fursa ya mbolea ya ruzuku inayotolewa na Serikali ili kuhakikisha wanalima kwa wingi zao hilo.

Awali wakulima wengi wadogo walishindwa kumudu kununua mbolea kutokana na bei kubwa lakini hivi sasa changamoto ya mbolea imekwenda kumalizika kutokana na serikali kutoa mbolea ya ruzuku kwa wakulima.

# CHUMA ULETE INAVYOWAKONDESHA WENGI

NA MWANDISHI WETU

WAKATI ikiwa ni kilio kikubwa juu ya "Chuma Ulete', kitu ambacho kinawakondesha wajasiriamali wengi, baadhi yao wanaamini kuna watu wanaishi maisha ya anasa na starehe bila kufanya kazi.

Wanaamini kuwa nguvu ya "Chuma Ulete' imesababisha madhara makubwa kwao, lakini imewafaidisha wao na wanawajua baadhi ya watu ambao wanatembea na 'bidhaa' hiyo mfukoni ili tu mambo yao yaende sawa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wachuuzi na wafanyabiashara walidai 'Chuma Ulete' ni aina ya mazingaombwe yanayofanywa na baadhi ya watu wanaoishi kwa kutofanya kazi kwa kuwaibia wengine kwa njia za Imani isiyofaa.

Mmoja kati ya wafanyabiashara hao, Sakina Abdallah anayeoka mikate katika eneo la Tandika, Dar es Salaam alisema kitu kinchoitwa 'Chuma Ulete' kinawatesa mno na kinawafanya wawe maskini wa kutupwa.

"Yaani ni balaa tupu, kama mimi nilipo hapa naweza kujikuta nimeuza sana lakini ikifika jioni sina kitu, unajiuliza hela imekwenda wapi kumbe watu wa "Chuma Ulete' wameshakupitia," alisema.

Katika mahojiano maalumu na uchunguzi uliofanywa na gazeti hili kwa kina ulibaini mambo mengi yaliyo na simulizi ya kusisimua juu ya kitu kinachoitwa 'Chuma Ulete' na kimesambaa miongoni mwa jamii ya Watanzania walio wengi.

USIKOSE MAKALA HAYA KWA KINA KATIKA TOLEO LETU LA JUMATATU, AMBAPO TUTAZUNGUMZIA KWA UNDANI JUU YA KITU HIKI KIITWACHO 'CHUMA ULETE'.



# NOTI MPYA KUANZA KUTUMIKA FEBRUARI MOSI

NA MWANDISHI WETU

GAVANA wa Benki Kuu ya Tanzania, Emanuel Tutuba amesema kuwa noti mpya za Tanzania zenye saini ya Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na yeye mwenyewe, za toleo la mwaka 2010, zitaingia kwenye mzunguko kuanzia Februari Mosi mwaka huu.

"Mheshimiwa Waziri, ninayofuraha kukujulisha kuwa zoezi letu la uchapaji upya wa Noti kwa marejeo ya toleo la mwaka 2010, limekamilika na tayari tumewajulisha wananchi kupitia taarifa niliyoitoa kupitia Gazeti la Serikali," alisema Tutuba.

Gavana Tutuba alifafanua kuwa noti hizo zitatumika sambamba na Noti zilizopo hivi sasa, zinamwonekano wa Noti zinazotumika hivi sasa zilizotolewa Mwaka 2010, ikiwemo alama za usalama, ukubwa, rangi na mambo mengine, isipokuwa ina marekebisho kwenye saini ya Waziri wa Fedha, na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania.

"Saini ya aliyekuwa Waziri wa Fedha ambaye hivi sasa ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Isdor Mpango imebadilishwa na kuwekwa Saini yako Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na Saini ya aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania aliyestaafu, Prof. Florens Luoga, imebadilishwa na kuwekwa Saini ya Gavana wa Benki Kuu wa sasa, Bw. Emmanuel Tutuba" aliongeza Tutuba. Akizungumza baada ya kupokea sampuli za Noti hizo mpya, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, alimshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu jambo hilo kufanyika na kumpongeza Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Emmanuel Tutuba, kwa kusimamia mchakato wa uchapaji wa Noti hizo kwa weledi na uadilifu mkubwa.

"Mpaka kufikia hatua hii ni heshima kubwa kwa Taifa letu na inaendeleza heshima ya wataalam wetu mnavyoweza kusimamia kwa umakini mambo yenye maslahi mapana kwa nchi yetu" Alisema Dkt. Nchemba.

Mhe. Dkt. Nchemba aliridhia Noti hizo ziingizwe kwenye mzunguko na kuanza kutumika kama ilivyopangwa tarehe moja Februari mwaka huu.

# BENKI KUU YANUNUA TANI 2.6 ZA DHAHABU

NA MWANDISHI WETU



WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde, amebainisha kuwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imenunua tani 2.6 za dhahabu inayochimbwa na kusafishwa hapa nchini ikiwa ni sehemu ya juhudi za kukabiliana na changamoto ya upungufu wa fedha za kigeni, kuboresha akiba ya fedha za kigeni, na kuimarisha thamani ya shilingi ya Tanzania.

Amesema hayo jana jijini Dodoma, wakati akiwasilisha taarifa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, taarifa inayohusu utendaji wa viwanda vya kusafisha dhahabu nchini kwa kipindi cha Machi hadi Desemba 2024 pamoja na mwenendo wa ununuzi wa dhahabu unaotekelezwa na BoT.

Kwa mujibu wa Waziri Mavunde, Oktoba 1, 2024, Tume ya Madini ilitoa tangazo linalowataka wachimbaji na wafanyabiashara wa dhahabu kutekeleza takwa la Kifungu cha 59 cha Sheria ya Madini Sura 123, ambalo linawataka kutenga asilimia 20 ya dhahabu na kuiuzia BoT kupitia viwanda vya usafishaji vilivyoidhinishwa.

"Mheshimiwa Mwenyekiti, Tangu kutolewa kwa tangazo hilo hadi Januari 21, 2025, BoT imefanikiwa kununua tani 2.6 za dhahabu kutoka kwa wachimbaji wa kati, wachimbaji wadogo, na wafanyabiashara wa dhahabu. Thamani ya dhahabu hiyo ni zaidi ya shilingi bilioni 570 kwa mujibu wa bei ya soko la dunia ya tarehe 22 Januari 2025" amesema Mavunde.

Waziri Mavunde amesisitiza kuwa, kupitia mpango huo wa BoT, lengo la Serikali ni kuifanya Tanzania kuwa moja ya mataifa 10 yenye hifadhi kubwa ya dhahabu barani Afrika kwa ustawi wa taifa.

Kwa upande wa mapato, Waziri Mavunde amebainisha kuwa, mwenendo wa ukusanyaji wa mrabaha kwa upande wa madini ya dhahabu umeendelea kuimarika na kwamba kuanzia Julai 1, 2024 hadi Desemba 31, 2024, Serikali iliingiza shilingi bilioni 400.22 kutokana na mauzo ya kilogramu 34,826.75 za dhahabu, ikiwa ni ongezeko la asilimia 5.55 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2023, ambapo kilogramu 32,995.54 ziliuzwa na Serikali kupata shilingi bilioni 278.86.

Katika hatua nyingine, Waziri Mavunde aligusia maendeleo ya Kiwanda cha Kusafisha Makinikia cha Tembo Nickel Refining Limited, kitakachojengwa Kahama, mkoani Shinyanga katika eneo ambalo awali lilikuwa likitumiwa na Mgodi wa Buzwagi, ambao umesitisha shughuli za uzalishaji wa dhahabu.

Amefafanua kuwa mradi wa Kiwanda hicho ni moja ya miradi machache barani Afrika inayozalisha bidhaa iliyotayari kwa matumizi, hivyo unatarajiwa kuleta tija kubwa kwa uchumi wa nchi, sambamba na kuimarisha Mchango wa Sekta ya Madini.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dkt. Mathayo David, amepongeza juhudi hizo na kueleza kuwa hatua hiyo itasaidia kuimarisha shilingi ya Tanzania, kuimarisha akiba ya dhahabu, na kuiweka nchi katika orodha ya mataifa yenye hifadhi kubwa ya dhahabu ulimwenguni.

Juhudi hizo ni sehemu ya mikakati ya Serikali kupitia Wizara ya Madini kuhakikisha kuwa Sekta ya Madini inatoa mchango mkubwa zaidi kwa uchumi wa Taifa na ustawi wa wananchi.

# KILIMO BIASHARA KITAKAVYOKUTOA



NA MWANDISHI WETU

KILA mara wakulima wanashauriwa kuweka kilimo katika mtazamo wa kibiashara. Wakulima wanaochukua na kuufanyia kazi ushauri huo, kisha kufanya shughuli za kilimo kitaalamu na kwa mtazamo wa kibiashara ,wanapata faida.

Kuwa na wazo ni aina gani ya kilimo unayoweza kuifanya kibiashara pekee haitoshi. Huo ni mwanzo tu. Ni lazima kukusanya au uwe na pesa au mtaji kwa ajili ya kugharamia shughuli hiyo na mwisho utakapouza bidhaa zako au huduma utakayotoa uweze kupata pesa zaidi. Hapo ndipo wazo la biashara linatekelezeka.

**Mpango wa biashara**

Unapoomba mkopo, ambapo kwa kawaida mkopeshaji ni benki na taasisi nyinginezo za fedha, utaulizwa mpango wa biashara yako unayokopea fedha hizo. Hata kama haujakopa au hauna nia ya kukopa pesa, kuelewa mpanga wako wa biashara ni muhimu. Inakuwezesha kujia unafanya nini na kama unachofanya kitaleta faida au unapoteza muda wako tu!

Mpango wa biashara unatoa tafsiri ya malengo yako katika mageuzi ya kibiashara. Kwa nini unafikiri malengo hayo yatafikiwa, na nini mikakati ya kuyafikia malengo hayo?

Kwa bahati mbaya wakulima wengi hawajaelimika katika kufanya shughuli zao za kilimo kibiashara na kuwa na mpango wa biashara. Bila kuwa na mpango wa biashara ni vigumu sana kuweza kumshawishi mtu au taasisi ya fedha kuwekeza katika mradi wako.

Mpango wa biashara hubadilika kulingana na ukubwa wa biashara unayolenga, utaalam utakaotumika, na ni nani walengwa katika mradi huo.

**Muhtasari wa wazo lako**

Lengo ni kutoa mtazamo mzima wa biashara husika na ushirika huo, unaelezea kwa ufupi biashara husika, bidhaa au huduma zitakazojumuishwa, uchambuzi wa soko la bidhaa au huduma hizo kwa ufupi, mikakati ya kupata soko na pia uchambuzi kwa ufupi ni jinsi gani fedha hizo zitasimamiwa kuahakikisha zinafanya shughuli lengwa.

Hii iwe wazi na ya kueleweka ili kutoa mtizamo mzuri wa biashara unayokusudia. Ni lazima uwe wazi kabisa kuelezea lengo la fedha unazokopa au kuomba. Muhtasari unaotoa ni lazima kuelezea kwa uhakika kuwa biashara yako itafanikiwa. Muda mzuri wa kuandika muhtasari ni baada ya kuandika mchanganuo wa biashara na kisha uunganishe mwanzoni mwa mpango wako wa biashara.

Wazo la biashara hutoa taarifa juu ya bidhaa utakazouza au huduma utakayotoa.

**Mpango wa soko**

Unajumuisha mambo yote unayofanya kutafuta wateja, ni nini wanachohitaji, na namna ya kuwafikia. Sehemu hii itaelezea bidhaa na huduma zako kwa undani, pia bei za bidhaa au huduma zako na ni wapi biashara ama ofisi yako itakapokuwa na mbinu utakazotumia kusambaza bidhaa zako.

**Mfumo wa biashara**

Hii inaelezea mfumo wa biashara yako kisheria, mfumo uliochagua unategemeana na faida na hasara ambazo kila sharia inazo. Uchaguzi huu unaweza kuwa wa mtu binafsi, ushirika au kampuni isiyokuwa na kikomo au ujamaa.

Katika sehemu hii, pia unatakiwa uoneshe ni kwa jinsi gani ulivyofikiria mahitaji ya kisheria na ni kwa jinsi gani umeweza kufuata katika utaratibu mzima wa kuanzisha biashara yako.

**Mipango ya fedha**

Unahitaji kuwa na bajeti. Sehemu hii itasaidia kuweza kupangilia faida na mtiririko mzima wa fedha katika biashara yako mpya. Hii ina maana ya fedha zinazoingia (mapato) na zinazotoka (matumizi). Ukishatengeza bajeti ni rahisi kutumia taarifa hiyo kufanya hesabu ya fedha unazohitaji kwa ajili ya kuanzisha biashara yako.

Huu unaitwa mtaji, na unatakiwa kuonesha chanzo cha mtaji huo. Hii ina maana ya kuonesha ni chanzo kipikitakachochangia asilimia flani katika fedha hizo.

**Angalizo**

Kuandika mpango mzuri wa biashara hakukuhakikishii kufanikiwa lakini ni njia moja wapo ya kupunguza uwezekano wa kuanguka kibiashara.

Kujaribu huleta mafanikio. Anza kuandika leo na upate uzoefu utakaokuletea mafanikio.



# UTUPA: MMEA UNAOFAA KWA MENGI

UTUPA ni aina ya mmea unaopatikana zaidi sehemu zenye baridi hasa nyanda za juu na unastawi sehemu zenye mvua za wastani na nyingi. Mmea huu hauhimili ukame.

Utupa hukua haraka na kusambaa kama usipodhibitiwa, baadhi ya nchi mmea huu umepigwa marufuku kupanda kwa sababu ya kutishia uoto wa asili.

Lakini una matumizi makubwa zaidi ambayo yanaweza kukushangaza na hata kukufurahisha na kama ulikuwa hujui unapaswa kulijua hili.

Kufukuza panya, mchwa

Mmea wa utupa ni moja ya njia za asili zinazotumika kufukuza wanyama na wadudu wa aina mbalimbali wanaoharibu mazao shambani.

Endapo shamba lako limevamiwa na panya wanaochimba ardhini, unaweza kupanda utupa kwa kuchanganya na mazao mengine.

**Nafasi**

Panda utupa pamoja na mazao mengine kwa umbali wa mita 3 kila upande (3m * 3m) na mpakani mwa shamba.

Baada ya kipindi cha mwaka mmoja shamba halitakuwa na mashimo ya panya wala fuko.

Njia hii pia itakuwezesha kufukuza mchwa, kwenye majumba. Unaweza kuupanda mmea huu kwenye kingo za nyumba na mpakani, kama kuna kichuguu cha mchwa panda miche hii na kichuguu kitakufa baada ya mchwa kuhama.

**Kuogeshea mifugo**

Unaweza kutumia mmea wa utupa kutengenezea mchanganyiko maalumu, ambao unaweza kuutumia kuogesha mifugo ili kuwakinga na kuwaondolea maradhi ya ngozi.

**Namna ya kuandaa**

Chukua kilo moja ya majani ya utupa na maji lita 25, loweka kwa saa mbili mpaka tatu au chemsha kwa dakika 30 na lita 27 za maji, chuja kwa kitambaa kisha weka kwenye bomba la kuogeshea mifugo, changanya na sabuni ya unga kidogo ili iweze kunata kwenye mwili wa mnyama, na hapo inakuwa tayari kwa matumizi.



Onyo

Kamwe usitumie kuogeshea nguruwe hawana uwezo wa kuhimili dawa hii kwenye ngozi zao.

Kunyuzia shambani, bustani

Utupa unaweza kutumika kwenye mazao ya aina mbalimbali, hii ikiwa ni njia mojawapo ya kukabiliana na wadudu waharibifu na magonjwa yatokanayo na wadudu hao.

**Namna ya kuandaa**

Chukua kilo moja ya majani ya utupa na maji lita 5 loweka kwa saa mbili mpaka saa tatu au chemsha kwa dakika thelathini na lita 6 za maji.

Chuja kwa kitambaa kisha weka kwenye bomba na kunyunyuzia shambani au majumbani kwa ajili ya kuua wadudu kama vile mbu, mende, n.k

Kuhifadhi nafaka kwenye ghala

Chukua gramu 100 za unga wa majani ya utupa changanya na mahindi au maharagwe kilo 100, funga vizuri gunia lako na hifadhi kwenye ghala. Dawa hii huwa na nguvu kwa muda wa mwaka mzima.

**Matumizi mengine**

Endapo utupa utapandwa mchanganyiko na mazao mengine huongeza rutuba ardhini kwa kuongeza kiasi na naitrojeni.

Mbegu zake zinaweza kutumika kama moja ya chanzo cha protini kwenye vyakula vya mifugo, hususani mbuzi.

**Tahadhari**

Usilishe kwa kiwango kikubwa kwani mbegu za utupa zina chembechembe za sumu zinazoweza kudhuru mifugo endapo zitaliwa kwa wingi.

Unga wa mbegu za utupa, unaweza kusababisha samaki wapooze (paralyze).

# WAMACHINGA
## WATU SAHIHI, KATIKA NCHI SAHIHI, KWA RAIS SAHIHI

UNAWEZA usijue umuhimu wa Wamachinga, lakini ukweli kada hiyo ni ya watu sahihi, ambao wapo katika nchi sahihi na wanaongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa mtu sahihi kwao kutokana na jinsi anavyowajali, kuwasikiliza na kutatua shida zao.

Kuonyesha jinsi anavyowajali, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan katika siku za nyuma ili kuondoa kero zilizokuwa zinawakabili, aliahidi kutoa Shilingi milioni 10 kwa ajili kutatua changamoto ya uendeshaji wa ofisi za Machinga mikoani.

"Nimesikia changamoto za uendeshaji wa ofisi na ninaahidi kutoa Sh milioni kumi kwa kila mkoa ili kutatua kero hiyo," alikaririwa Rais Dkt. Samia, akitoa ahadi hiyo kipindi hicho.

Katika kuwawekea mazingira mazuri, mbali na kuwarahisishia kupata mikopo, pia Rais Dkt. Samia aliagiza mamlaka husika za usimamizi wa fedha, kutengeneza mifumo mizuri ili tu waweze kupata mikopo kirahisi na kuendesha biashara zao.

Hayo yalionekana na kuthibitishwa na Chama cha Wafanyabiashara Ndogondogo Mkoa wa Dar es Salaam (KAWASSO) ambapo walisema kuna mwanga mpya wa fursa kupitia kwa wadau wa Banki Maendeleo kwa kuwakopesha.

Benki hiyo inatarajiwa kuwafikia Wamachinga zaidi ya elfu tano, pamoja na makundi ya Wanawake na vijana kuwapatia Elimu ya Biashara na kuwapatia mikopo yenye riba nafuu kwa wale wanaokidhi vigezo ili kuweza kuwainua kiuchumi.

Pia imeweza kuwapatia mikopo ambapo imewafikia Wamachinga 1800 kwa mwaka jana kusababisha kuinua uchumi wa kila mmoja.

Baadhi ya maeneo yanayoendelea kufikiwa na mikopo hiyo ni Solo la Kariakoo, Machinga Complex, Soko la Bog Brother, SoKo la Feri, Maeneo ya Tabata Muslim.

Maeneo mwengine ni Tazara Vetenary ambapo imetajwa kuwa kila mmoja aliyepata mkopo huo kwa mwaka jana pia alikuwa tayari amekata Bima ya kujilinda na majanga endapo itatokea ajali ya moto katika bidhaa zake.

Ukweli ni kwamba Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa akitoa maelekezo maalum ya kuweza kuyalea makundi ya machinga na bodaboda.

Katika moja ya hotuba zake, Waziri Mkuu wa Tanzania, Kassim Majaliwa alisema Wamachinga ni watu muhimu katika kukuza pato la Taifa na takwimu za Wizara ya Viwanda na Biashara zinaonesha kuwa Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo imetengeneza ajira, kukuza uchumi na kuondoa umasikini.

Hivyo, Waziri Mkuu aliziagiza mamlaka zinazohusika na ujenzi wa masoko mazuri unaoendelea kwenye maeneo mbalimbali nchini wazingatie na waandae miundombinu kwa ajili ya wafanyabiashara ndogo ndogo maarufu kama wamachinga.

Waziri Mkuu amesema kuona Wamachinga kama ni fursa ya uchumi utekelezaji wake utakuwa ni mwarobaini wa changamoto zote zinazowakabili Wamachinga nchini kwani kila mmoja kwa nafasi yake atatimiza wajibu wake ili kuhakikisha wanafanya kazi zao na hivyo kuweza kuchangia ujenzi wa uchumi wa Taifa.

Alisema anaamini kuwa wadau wote nchini watashirikiana katika kuchochea maendeleo ya wafanyabiashara wadogo kwa kuweka mazingira bora ya kufanya biashara na hivyo kuwawezesha kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja na pato la Taifa kwa ujumla.

Waziri Mkuu alisisitiza kwamba Wamachinga ni watu muhimu sana na wamekuwa suluhisho la mahitaji kwa watu wengi kuanzia wenye kipato cha chini, kati na kipato cha juu, hivyo ametoa rai kwa Watanzania wote kuendelea kuunga mkono shughuli zao kwa vitendo

Pia, Waziri Mkuu alisema Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wamachinga wote nchini ikiwa ni pamoja na kuwapatia vitambulisho maalum vinavyowapa uhalali wa kufanya biashara zao bila bugudha.

"Napenda kuwahakikishia kwamba Serikali inathamini sana mchango mkubwa wa sekta isiyo rasmi katika kuinua uchumi." Amesema, "Wakurugenzi katika Halmashauri zote wahakikishe wanapata takwimu sahihi za Wamachinga ili irahisishe zoezi la utoaji vitambulisho vya biashara ili kuepuka usumbufu.

"Ndugu zangu Wamachinga vitambulisho ni muhimu kwani vinakupeni uhalali wa kufanya biashara zenu bila bugudha."

Alisema hata sekta zilizo rasmi nao wana vitambulisho vinavyowawezesha kupata huduma zao kama waajiriwa. Serikali imeamua kutoa vitambulisho rasmi ambayo vitawatambulisha popote nchini na kupata huduma muhimu.

Waziri Mkuu alisema sekta isiyo rasmi imetoa fursa nyingi za ajira ikilinganishwa na wale walioajiriwa katika sekta rasmi. "Kwa kutambua hilo, nitoe wito kwa wamachinga wote kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kuchangia ukuaji wa pato la Taifa."

Alisema Sekta ya Biashara Ndogo imesaidia kutatua changamoto ya ukosefu wa ajira nchini kwani imewezesha kila mpenda kazi kwa vijana, wanawake na wahitimu wa ngazi zote kujiajiri ikiwemo wanaohitimu wa elimu ya msingi, sekondari, ngazi ya kati na hata vyuo vikuu.

Waziri Mkuu alisema, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kushughulikia changamoto zinazowakabili Wamachinga ikiwa ni pamoja na kuwajengea mazingira bora yatakayowawezesha kufanya biashara zao katika maeneo stahiki.

Waziri Mkuu, pia alitumia fursa hiyo kuwataka Wamachinga wawe wazalendo na wasikubali kutumika kwa kusaidia mtu mwingine kukwepa kulipa kodi kwa kukubali kupokea bidhaa kutoka katika maduka makubwa bila risiti ya mauzo kitendo ambacho kinasaidia kutolipa kodi, hivyo, aliwataka wasikubali kusaidia wafanyabiashara wakubwa kukwepa kodi wakati wao wanalipa kodi.









# MBINU MUHIMU WAKATI WA UANZISHAJI UFUGAJI WA SAMAKI

**UNAPOTAKA kufuga samaki ni lazima ujiandae kwanza na hapa tunajaribu kukuletea mambo ambayo unapaswa uyafuate kabla ya kuanza kuwa mfugaji wa samaki na uwe na matokeo bora yatakayokuwezesha kuwa na mafanikio makubwa.**

Kwanza kabla ya kuamua kuwa mfugaji wa samaki, unatakiwa uwe na shauku na dhamira ya kweli ya ufugaji, kufanya tathmini ya rasilimali ulizonazo kwa ajili ya mradi wa ufugaji wa samaki.

Pia lazima uwe na uhakika wa chanzo endelevu cha mtaji kwa ajili ya mradi, hulka ya uvumilivu na kuthubutu, tathmini ya soko la bidhaa za samaki na kujipatia maarifa ya msingi ya ufugaji wa samaki.

### ENEO LA KUFUGIA

Eneo la kufugia samaki linatakiwa liwe na maji ya kutosha kwa mwaka mzima, linatakiwa liwe na udongo unaoweza kutuamisha maji, lisiwe na historia ya mafuriko, kwa kuwa mafuriko yakitokea samaki waliokuwa bwawani wataondoka na maji na bwawa litafunikwa na udongo.

Pia eneo zuri la kufugia samaki ni lile linalofikika kwa urahisi, linatakiwa kuwa ni eneo lenye amani na utulivu na watu wenye

Kuelewana, kuwa na soko la bidhaa na umiliki wa ardhi wa uhakika.

### BWAWA

Zipo namna mbalimbali za utengenezaji wa bwawa la samaki, kulingana na aina ya bwawa lenyewe, hali ya uchumi, wingi wa samaki pamoja na aina ya samaki watakaofugwa.

Hapa najaribu kuwaonyesha aina za mabwawa ya kufugia

Samaki, ambapo ni bwawa la kuchimba udongo bila kujengea na lile la kuchimba udongo na kujengea kwa matofali, simenti na zege.

### UANDAAJI NA UPANDIKIZAJI

Kabla ya kuvisafirisha vifaranga kutoka kwenye bwawa wanaloishi ni vema vikatolewa na kuwekwa kwenye vibwawa vidogo vidogo kwa muda wa kati ya saa 24 hadi 72 (kutegemeana na umbali wa safari) bila chakula.

Wakati wa kupandikiza mfugaji anatakiwa akifika asivimwage vifaranga kwenye bwawa bali anatakiwa kuyaruhusu maji yaliyobeba vifaranga yabadilishane ujoto na maji yatakayopokea vifaranga.

Hapa mfugaji anatakiwa kuliweka kontena au chombo alichobebea vifaranga kielee kwenye maji anayotaka kufugia kwa muda wa dakika kati ya 30 hadi 35, baada ya hapo chombo

kilicho na vifaranga kifunguliwe na kiinamishwe ili maji hayo yaweze kukutana na yale yaliyoandaliwa kwa ajili ya kufugia na hapo ataruhusu vifaranga kuingia wenyewe kwenye bwawa husika.

Iwapo utafika na kuvimwaga vifaranga kwenye bwawa jipya bila kufuata utaratibu huo wa kitaalamu basi tofauti ya ujoto wa maji kati ya chombo kilichosafirishiwa vifaranga na bwawa unaweza kusababisha vifaranga wote kufa kwa muda mfupi, kitaalamu wanasema kuwa vifo vya vifaranga hivyo vinasababishwa na mshituko wa joto.

Jambo lingine la kuzingatia ni kuwa uandaaji na usafirishaji wa vifaranga ni vizuri ukafanywa muda ambao hali ya hewa inakuwa na ubaridi. Muda unaopendekezwa zaidi na wataalamu ni asubuhi au jioni kwa sababu muda huo samaki wanakuwa na uwezo wa kuhimili misukosuko ya safari tofauti na hali ya hewa inapokuwa ya joto.

UFUGAJI KIANGAZI, MASIKA

Kimsingi hakuna tofauti kubwa wala athari kubwa sana za ufugaji wa samaki wakati wa kiangazi ukilinganisha na wakati wa masika, tofauti zilizopo ni ndogo ndogo ambazo kitaalamu hazina madhara makubwa kwa mfugaji.

Hii ni ulaji wa chakula wa samaki na ukuaji wao na uchafuzi wa maji yanayoingia kwenye mabwawa ya kufugia

### ULISHAJI NA UTUNZAJI

Samaki wapewe chakula angalau mara 2 kwa siku (saa 3-4 asubuhi na 9-10 jioni) pia kuwe na hewa ya kutosha, kuwapa vyakula tofauti kutegemeana na silka ya aina ya samaki unaowafuga.

Kuna samaki wanaofaidika na vyakula vya nyama nyama kama vile kambale na sangara (hawa hawali pumba) na kuna samaki wengine kama sato wanakula vyakula mchanganyiko wa nyama na

mboga mboga na wapo wengine wanaokula vyakula vyenye asili ya mimea tu.

Kuhusu maji hapa ifahamike kuwa wakati tunazunguzia viwango vya maji vinavyohitajika kwa wanyama wengine wafugwao, hitaji la maji kwa samaki ni ubora wa maji anayofugiwa na sio wingi wake.

### MASOKO YA SAMAKI

Soko la awali, hili ni soko la moja kwa moja kutoka kwa muuzaji ambaye ni mfugaji kwenda kwa mlaji, kuna soko la kati, katika soko hili kwa kawaida kunakuwa na mtu wa kati ambaye ananunua samaki kwa mfugaji kwa lengo la kwenda kuwauzia walaji.

Soko la kimataifa, hili ni soko linalofanyika nje ya nchi (baina ya nchi moja na nchi nyingine).

# DK. SAMIA ALIVYOPIGA 'HAT–TRICK' KATIKA UWEKEZAJI, MIFUGO

NA CHARLES MATESO

KATIKA soka wanasema 'hat-trck', ikiwa na maana kafunga mabao matatu katika mchezo mmoja husika. Ukishapiga 'hat-trick yako na kwa heshima ya mchezo, unapewa mpira unauweka kwapani na kuondoka nao.

Hivyo ukitzama kinachoendelea katika sekta mbili tu za mifugo na utalii, unaweza kutamka bila kusita, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameupiga mwingi, kapiga 'hat-trick' na mpira kabeba kabisa.

Ni data tu zinazungumza kuhusu kile kinachofanywa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika sekta hizo mbili ambazo zimebeba mamia ya watu wanaozitegemea huku zikiwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa.

**MIFUGO**

Ukitazama katika mifugo, ameendelea kufanya kweli kwa Watanzania baada ya kutoa kiasi cha Sh Bilioni 28.1 katika sekta ya mifugo ili kutekeleza mapinduzi makubwa katika mifugo.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi Dkt. Ashatu Kijaji, amethibitisha hilo na kusema, Serikali ya Awamu ya Sita imetenga fedha Shilingi Bilioni 28.1 kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 kwa ajili ya sekta ya mifugo pekee ili kutekeleza mapinduzi ya sekta hiyo ikiwemo kufanya kampeni ya chanjo ya mifugo ili kuhakikisha mifugo hapa nchini inakuwa na ubora unaohitajika kimataifa.

Waziri Dkt. Ashatu Kijaji amesema, fedha hizo zimelenga kutoa chanjo za homa ya mapafu ya ng'ombe, ugonjwa wa sotoka ya mbuzi na kondoo na ugonjwa wa kuku wa kideli huku fedha nyingine kutumika kununua pikipiki 700 na vishikwambi 4,500 kwa ajili ya maafisa ugani wa mifugo ili kurahisisha utendaji kazi wao hivyo kutimiza maono ya Rais Dkt. Samia.

"Kwa mara ya kwanza ndani ya miaka 60 tangu tupate uhuru, Mama (Dkt. Samia) katupa Shilingi Bilioni 28.1 kwa ajili ya wafugaji tu..." amesema Dkt. Ashatu Kijaji.

Hivyo wafugaji wametakiwa kwenda na kasi ya mapinduzi ya sekta hiyo na kutekeleza kwa vitendo utaalamu wanaopewa na maafisa ugani kwani Dkt. Samia Suluhun Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ana dhamira ya dhati ya kuhakikisha mapinduzi ya sekta hiyo yanafanikiwa.

Pia Serikali nchini kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imewahakikishia wafugaji kuwa hakuna mifugo itakayopotea kutokana na magonjwa mbalimbali.

Madhumuni ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuhakikisha nchi inakuwa na mifugo mizuri yenye kuleta tija kwa wafugaji na wawekezaji wa nyama, hivyo wafugaji waiamini serikali kwa jinsi inavyowapambania katika kuhakikisha soko la bidhaa hiyo inakuwa kubwa na yenye tija kwao.





**UWEKEZAJI**

Katika uwekezaji, Tanzania imezidi kupaa huku ikielezwa yote hayo yanatokana na jitihada za dhati zinazofanywa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Hii inathibitishwa na miradi 500 ya uwekezaji iliyosajiliwa mwaka 2023 wakati ndani ya mwaka 2024 imesajiliwa miradi ipatayo 901.

Kubwa zaidi wakati miradi 500 ya mwaka 2023 ilikuwa na thamani ya dola za kimarekani bilioni tano, miradi 901 iliyosajiliwa mwaka 2024 ina thamani ya dola za kimarekani bilioni 9.3.

Hayo yamethibitsihwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo Cha Uwekezaji Nchini (TIC), Dk. Binileth Mahenge aliyesema mwamka wa usajili wa miradi ya wawekezaji umeongezeka kutokana na fursa zinazotolewa na Rais Dk. Samia.

Kwa hilki, Dkt. Samia ataendelea kuupiga mwingi tu na zile 'hat-trick' katika sekta nyingine zitaendelea.



# UMUHIMU WA KUHIFADHI NAFAKA



**Ni wazi kuwa wakulima wengine wamevuna nafaka mbalimbali kama vile maharage na mahindi katika msimu huu wa mavuno hivyo wasipokuwa makini na kuhifadhi kwa usahihi mavuno yote yatapotea kwa kuharibiwa na wadudu, panya, au hata ukungu unaotokana na unyevu.**

Ili kuepukana na hasara ni muhimu kuhakikisha unahifadhi mazao yako katika njia salama kama unavyoshauriwa na Mkulima Mbunifu au wataalamu wa kilimo.

Kabla ya kuhifadhi hakikisha mazao yako yamekauka vizuri kwa kung'ata punji ambayo huwa ngumu na hukatika kwa mlio mkali, kumimina kwenye chombo au sakafu, ambapo hutoa mlio mkali kama wa kuumiza sikio, kutumia chumvi yaani kuchanganya mahindi na chumvi kiasi kisha mimina kwenye jagi la kioo, na kama chumvi itang'ang'ania kwenye punje basi hazijakauka au kutumia kipima unyevu ambacho huonyesha unyevu wa asilima 13.5.

**KABLA YA KUHIFADHI**

Kabla ya kuweka nafaka kwenye vifungashio au kuhifadhi ghalani, inabidi kuchukua tahadhari ya kuzuia uharibifu utokanao na wadudu au wanyama kama panya ndani ya ghala.

Hakikisha ghala la kuhifadhia nafaka ni safi, lisilovuja na ikibidi changanya mahindi na viuwadudu.

Viuwadudu hivyo vinaweza kuwa vya asili vinavyotokana na mimea kwa mfano mwarobaini au pareto. Aidha ni muhimu kutenga kiasi cha nafaka itakayotumika kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu baada ya kuvuna. Hii ni kwasababu katika kipindi hiki, mashambulizi ya wadudu huwa ni ya kiwango cha chini sana.

**Kuchanganya kiuwadudu na nafaka**

Wakati wa kuchanganya kiuwadudu na nafaka ni muhimu kuandaa vifaa kama vile, turubai isiyokuwa na matundu, sakafu safi ya sementi, debe la kupimia nafaka, beleshi au koleo, dawa ya kuhifadhia na kifaa au kitambaa safi cha kufunika pua na mdomo.

**Hatua za kuchanganya**

Tandika turubai safi kwenye sakafu katika sehemu isiyokuwa na upepo. Pima nafaka kwa kutumia debe au kwa kutumia mizani ili kupata uzito wa kilogramu 100 (madebe sita).

Weka nafaka kwenye turubai na funika pua na mdomo kwa kitambaa safi ili kuzuia dawa isiingie mwilini.

Fungua pakiti ya gramu 200 ya dawa ya asili na mimina juu ya kilo 100 za nafaka. Anza kuchanganya dawa nanafaka kwa kutumia beleshi au koleo mpaka mahindi yote yatakapopata dawa.

Fungasha kwenye magunia safi ya kilo 100 tayari kwa kuhifadhi ghalani au waweza kuhifadhi kwenye kihenge, silo au bini.

Nafaka zipangwe kimadaraja kwenye ghala. (Maguniua yasiwekwe moja kwa moja sakafuni, mbao huweza kutangulizwa sakafuni kwanza).

**Ghala bora**

Ghala bora ni chombo chochote kile au jengo lolote lililo imara na lenye sifa zifuatazo; Liwe na uwezo wa kuzuia wadudu, panya, mvua na unyevu kutoka chini.

Liwe na nafasi ya kutosha kuweka mazao, kukagua na kutoa pamoja na uwezo wa kuhifadhi mazao yaliyokusudiwa.

Aina ya maghala bora

**1. Sailo au bini**

Haya ni maghala yanayojengwa kwa dhana ya kutokuwepo na mzunguko wa kawaida wa hewa ndani ya nafaka iliyohifadhiwa na kusababisha wadudu waharibifu na vimelea vya magonjwa kutoweza kusitawi na kuharibu nafaka.

**2. Mapipa**

Mapipa yenye mifuniko imara hutumika kuhifadhi nafaka kwa dhana ya kutokuwa na hewa ndani ya mahindi. Pipa likijazwa mahindi na kufungwa sawasawa hakuna hewa inayoingia na hakuna mdudu anayeweza kuishi ndani yake, na hata punje za nafaka hufa baada ya kuhifadhiwa kwa muda hivyo inashauriwa kuwa nafaka inayotegemewa kwa ajili ya mbegu isihifadhiwe ndani ya pipa.

**4. Maghala ya nyumba**

Hifadhi hii hufanyika katika chumba au nyumba maalumu na maghala haya huhifadhi mazao yaliyofungashwa kwenye magunia. Uwezo wa kuhifadhi hutegemea wingi wa mazao.



# UKIWA MJASIRIAMALI JIFUNZE KANUNI HIZI

**WENGI hutamani au hata kujiingiza kwenye ujasiriamali, lakini siyo wote wanaofanikiwa kutokana na kutokufahamu kanuni muhimu za ujasiriamali. Ni wazi kuwa ili uanzishe kitu chochote chenye mafanikio, ni lazima ufahamu kanuni za kukifanya kitu hicho jinsi ipasavyo.**

Ikiwa wewe ni mjasiriamali, au unataka kuwa mjasiriamali, basi fuatilia makala hii ili nikufahamishe kanuni 13 za ujasiriamali.

**1. Kuwa mtatuzi wa matatizo**

Ujasiriamali ni zaidi ya kupata pesa, ni lazima kwanza utatue changamoto ya mtu ndipo utaweza kupata pesa kutoka kwa mtu husika. Ni muhimu ukafahamu kanuni hii kama mjasiriamali kwani hutojikita kutafuta pesa bali utajikita kutatua matatizo ya watu.

Kwa mfano kama kuna tatizo la upatikanaji wa mboga katika mji au eneo unalokaa, ikiwa wewe utaleta mboga katika eneo hilo ni wazi kuwa watu watakupa pesa ili uwape mboga. Hivyo ni muhimu kila mara ukatafuta changamoto ukaitatua, nawe bila shaka utapata pesa za uhakika.

**"Pesa ni matokeo ya kutatua shida ya mtu"**

**2. Kuwa na maono**

Hakuna ujasiriamali bila maono. Kuwa mjasiriamali bila maono ni sawa na kuendesha gari isiyokuwa na usukani. Maono katika ujasiriamali yatakuwezesha kukuongoza ufanye nini na kwa muda gani. Ni lazima ujiulize kuwa unataka kuwa nani, lini na unataka kufanya nini baadaye? Jonathan Swift alisema maono ni sanaa ya kuona kile ambacho wengine hawaoni. Ni lazima uwe na lengo na ufanye bidii kulifikia.

"Wajasiriamali waliofanikiwa ni wale walioweza kubadili maono yao kuwa uhalisia"

**3. Chagua washirika au timu sahihi**

Wakati mwingine utahitaji kufanya kazi na watu au mtu fulani. Ni muhimu kuwa makini wakati wa kuchagua washirika au timu ya kufanya nayo kazi ili kuhakikisha maono yako hayakwamishwi.

Kamwe usichukue mtu tu kwa kigezo kuwa ni rafiki au ndugu yako, bali chukua mtu ambaye unaamini anaweza kufanya kitu chenye tija kwa ajili ya kufanikisha malengo yako kama mjasiriamali.

**4. Toa huduma au bidhaa yenye tija**

Hivi leo sokoni kuna bidhaa na huduma nyingi ambazo ni za aina moja, lakini siyo zote zinafanya vizuri. Hii ni kutokana na baadhi ya bidhaa au huduma kutozingatia kuwa na tija kwa wateja wake. Ikiwa unatengeneza bidhaa au huduma fulani hakikisha itakuwa na manufaa makubwa na ya uhakika kwa wateja wako.

Kwa mfano nimewahi kuona vitafunwa vilivyoandaliwa katika mazingira duni na kuwa na dosari mbalimbali kama vile marashi, vipande vya nywele, mchanga n.k. Ni wazi kuwa bidhaa za namna hii zitakosa wateja kutokana na kuwa na ubora duni.

Kila mara kumbuka kuwa ushindani ni mkubwa, hivyo jitahidi kuongeza tija na ubora wa huduma na bidhaa zako.

**5. Fahamu na jali wateja**

Ikiwa wewe ni mjasiriamali, basi futa mawazo kuwa wateja wa nakuhitaji wewe. Fahamu kuwa wewe kama mjasiriamali, ndiye unaye wahitaji wateja ili ukuze biashara au huduma yako. Hakikisha mambo haya kuhusu wateja:

Fahamu wanataka nini, sikiliza maoni na ushauri wao, hakikisha unakamilisha mahitaji yao, tumia lugha nzuri na rafiki kwa wateja, mfanye mteja aone unamthamini, mfanye mteja aone kuwa umetanguliza huduma kabla ya pesa, naamini kwa kufanya hivi utaweza kujijengea msingi mzuri wa wateja kwa ajili ya huduma au bidhaa zako kila siku.

**6. Tumia pesa vyema**

Changamoto ya matumizi mabaya ya pesa inawakabili watu wengi kuanzia kwenye matumizi yao binafsi ya pesa. Watu wengi wanapata pesa lakini zinaisha bila ya kufahamu wamezitumiaje au wamefanya kipi chenye tija.

Ni wazi kuwa matumizi mazuri ya pesa ni kanuni muhimu sana kwa mjasiriamali, kwani kwa njia hii utaweza kukuza biashara yako kila siku. Jifunze kufahamu hii ni pesa kwa ajili ya nini, na uitumie kwa mambo ya msingi pekee. Epuka tabia za kibadhirifu na anasa. Ikiwa biashara au uwekezaji wako ni mkubwa, basi unaweza kumwajiri mtu aliye na taaluma ya utunzaji na usimamizi wa pesa.

**7. Usipuuze nafasi ya teknolojia**

Tunaishi kwenye ulimwengu wa sayansi na teknolojia, hivyo wewe kama mjasiriamali huwezi kujitenga nao. Kwa kupitia teknolojia kama vile simu na mtandao wa intaneti, unaweza kuwafikia watu wengi zaidi na kuongeza mauzo ya huduma au bidhaa zako.

Hakikisha wewe kama mjasiriamali unakuwa karibu na wateja wako ili kutatua shida na mahitaji yao; pia hakikisha unajifunza mbinu bora za kufanya biashara kupitia mtandao.

**8. Fahamu soko**

Kanuni mojawapo ya kuongeza mauzo yako kama mjasiriamali ni kulifahamu soko vyema. Hakikisha huduma au bidhaa unayoitoa inakidhi mahitaji na inafika kwenye soko stahiki.

Kwa mfano ikiwa wewe ni mzalishaji wa mayai, lakini eneo ulilopo soko ni duni, basi tafuta eneo jingine ambalo soko la bidhaa hii ni nzuri. Ikiwa wewe huwezi kwenda, unaweza kutafuta mtu kwenye eneo lenye soko zuri akakuuzia bidhaa yako na ukampa gawio fulani.

Kwa kufanya hivi utaweza kulenga soko na kujiongezea faida zaidi wewe kama mjasiriamali.

**9. Ongeza maarifa**

Kwanza nikupongeze kwa kusoma makala hii, ni wajasiriamali wachache sana ndiyo hupenda kusoma makala na vitabu mbalimbali ili kuongeza maarifa.

Ni muhimu sana kila mara ukajizoesha kujiongezea maarifa, hasa ya ujasiriamali pamoja na kile unachokifanya; hili liitakuwezesha kuwa na tija na kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Unaweza kusoma vitabu, majarida na tovuti mbalimbali (kama fahamuhili.com) ili kuongeza maarifa yako.

10. Jifunze kutokana na makosa

Moja ya kanuni inayozingatiwa na wajasiriamali waliofanikiwa ni kujifunza kutokana na makosa. Makosa ni shule nzuri sana kwa kila mtu hasa wajasiriamali. Ikiwa uliwekeza ukapata hasara, basi jifunze nini hasa kilikuwa chanzo cha hasara ili mbeleni uweze kukiepuka. Usikubali kukwamishwa na makosa, bali yawe ni hamasa kwako ya kuendelea mbele zaidi.

"Uzoefu ni kufanya makosa na kujifunza kutokana na makosa hayo"

**11. Tumia muda vizuri**

Hakuna mtu mwenye zaidi ya saa 24 duniani; lakini mwingine muda unamtosha wakati mwingine analalamika muda haumtoshi. Ni wazi kuwa mpangilio au matumizi mabaya ya muda ndiyo husababisha changamoto hii. Wewe kama mjasiriamali ni muhimu ukaondoa mambo yasiyokuwa na ulazima kwenye ratiba yako. Tambua ni kitu gani ni cha muhimu zaidi na ukifanye kwa wakati.

**12. Weka vipaumbele**

Wewe kama mjasiriamali, ni muhimu kuzingatia kanuni hii ya kujiwekea vipaumbele; vipaumbele vitakuwezesha kubaini ni kipi kianze na ni kipi kifuate kutokana na umuhimu wake.

Kwa mfano ikiwa kuna wateja walipata shida kupata huduma au bidhaa yako, maliza kwanza swala hili kabla ya kuendelea kuweka jitihada za kuuza bidhaa mpya. Kwa kufanya hivi utaweza kufanya mambo kutokana na umuhimu wake, jambo ambalo litakuwezesha kukua.

**13. Usikate tamaa**

Ni wazi kuwa katika safari ya ujasiriamali utakutana na changamoto mbalimbali. Jambo la msingi ni kukumbuka kanuni hii kuwa usikate tamaa. Tumia changamoto kama chachu ya kukuhamasisha kufanya bidii zaidi na usirudi nyuma.

Changamoto zipo leo na kesho lakini keshokutwa hazitakuwepo tena; jambo unalotakiwa kufanya ni kutazama lengo lako na kufanya bidii kila kukikucha kuzikabili changamoto husika ili ufikie lengo lako.

"Siri ya mafanikio yetu ni kutokukata tamaa"



# MABILIONEA WALIVYOZIDISHA UTAJIRI WAO 2024



SHIRIKA la kimataifa la kupambana na umasikini, Oxfam limesema siku ya Jumatatu kuwa utajiri wa mabilionea uliongezeka mara tatu zaidi mwaka uliopita wa 2024.

Shirika hilo la Oxfam limesema utajiri wa mabilionea ulikua kwa dola trilioni 2 mwaka jana, ikiwa ni sawa na takriban dola bilioni 5.7 kwa siku, ikiwa ni mara tatu zaidi kuliko mwaka 2023.

Idadi ya mabilionea iliongezeka kwa kuibuka mabilionea 204 na hivyo kupelekea idadi hiyo kufikia hadi 2,769, huku watu 10 ambao ni matajiri zaidi duniani wakishuhudia utajiri wao ukiongezeka kwa wastani dola milioni 100 kwa siku. Oxfam ilitumia chapisho la mwezi Novemba la jarida la Forbes linalowaangazia mabilionea wakubwa duniani.

Utafiti huu wa Oxfam unaipa uzito kauli iliyotolewa wiki iliyopita na rais wa Marekani anayemaliza muda wake Joe Biden ambaye alitahadharisha kuhusu mkusanyiko hatari wa mamlaka mikononi mwa matajiri wachache. Ripoti ya kundi hilo yenye jina la "Takers Not Makers,"ikizingatia takwimu za Benki ya Dunia, inaeleza pia kuwa idadi ya watu maskini wanaoishi na chini ya dola 6.85 kwa siku haijapungua tangu mwaka 1990.

Mitabh Behar, Mkurugenzi mtendaji wa Oxfam International, amesema katika mahojiano kuwa kuingia madarakani kwa Trump akisaidiwa na mshauri wake Elon Musk kunatoa picha ya kwamba kundi la matajiri wakubwa duniani ndiyo wanashikilia usukani wa uongozi.

Ameongeza kuwa hilo halimhusu mtu mmoja lakini ni mfumo wa kiuchumi ulioundwa ambapo sasa mabilionea wanaweza kuunda sera za kiuchumi na kijamii ambazo hatimaye huwanufaisha zaidi.

Sambamba na wito wa Biden wa kuwataka mabilionea waanze kulipa kodi na ushuru unaofaa, shirika la Oxfam limetoa wito kwa serikali za mataifa mbalimbali kuwatoza ushuru zaidi matajiri ili kupunguza hali ya ukosefu wa usawa na kukabiliana na utajiri uliokithiri.

Shirika hilo limetoa wito wa kuchukuliwa hatua kama vile kuondoa ukiritimba, kudhibiti malipo ya wakurugenzi watendaji, na kuhakikisha mashirika yanawalipa wafanyakazi mishahara stahiki.

Mwaka 2024, wawekezaji wengi walipata faida kubwa, hasa kutoka kwenye makampuni makubwa ya teknolojia, faharisi za soko la hisa, bei ya dhahabu na hata sarafu za mtandaoni. Oxfam imeendelea kuwa kwa wastani nchi zenye kipato cha chini na cha kati hutumia karibu nusu ya matumizi ya bajeti zao za kitaifa ili kulipa madeni.

Bango ka kongamano la kimataifa la kiuchumi la Davos, UswisiBango ka kongamano la kimataifa la kiuchumi la Davos, Uswisi.

Ripoti hiyo ya Oxfam imetolewa wakati wa ufunguzi wa kongamano la kimataifa la kiuchumi litakaloanza leo hadi Ijumaa huko Davos, shirika la Oxfam International katika tathmini yake ya hivi punde kuhusu hali ya ukosefu wa usawa duniani, limetabiri kuwa angalau matrilionea watano wataibuka katika muongo ujao.

Watu wapatao 3,000 wakiwemo wadau wa biashara, wasomi, viongozi wa serikali, na wawakilishi wa vikundi vya kiraia wanatarajia kuhudhuria kongamano hilo la kila mwaka katika mji wenye milima wa Davos nchini Uswisi.

Rais mteule wa Marekani Donald Trump, ambaye alihudhuria mara mbili kongamano la Davos wakati wa muhula wake wa kwanza, anatarajiwa mara hii kushiriki kwa njia ya video siku ya Alhamisi. Kwa muda mrefu, Trump aliyekula kiapo Jumatatu amekuwa akitetea suala la kujilimbikizia utajiri huku akimteua bilionea Elon Musk kama mshauri wake. Kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, waandamanaji kadhaa wameshuhudiwa huko Davos wakidai uwepo hatua za kiuchumi, kuwatoza ushuru matajiri na kushinikiza madai mengine yanayotetea usawa wa kijamii.

# SINDIKA TOGWA LIKUPE FEDHA

TOGWA ni kinywaji cha asili kinachonyweka kwenye maeneo mengi Tanzania pamoja na nchi zingine lakini ikitumika zaidi katika maeneo ya wakulima.

Kinywaji hiki chenye asili ya ubaridi kinatengenezwa kwa kutumia nafaka kama vile mahindi, ulezi, mtama (isipokuwa ngano) japo inasadikika pia kuwa kuna maeneo mengine wanatengeneza kwa kutumia matunda.

Asili ya togwa hapa nchini inasadikika kuwa imetokana na wanajamii wa kibantu ambao kwa miaka ya nyuma walikuwa wakijishughulisha na kilimo.

Togwa hutumika wapi

Kinywaji hiki cha baridi ambacho hunywewa na wa watu wa rika zote hutumika kama kiburudisho wakati wa kulima/kuvuna, kwenye sherehe za kijamii, kiasili, kikabila na hata wakati wa kazi zingine mbalimbali za kijamii.

**Usindikaji wa togwa**

Togwa inayotokana na ulezi pamoja na mtama, inaweza kusindikwa na kuhifadhiwa kwenye vyombo au chupa maalumu kisha kuuzwa kama bidhaa zingine sokoni.

Malighafi

Katika usindikaji huu, malighafi inayohitajika ni ulezi, mtama, maji, kimea pamoja na kilinda chakula (preservatives).

**Vifaa**

Hivi ni pamoja na sufuria, jiko, majaba, chupa maalumu za kuhifadhia, pamoja na karatasi/nailoni maalumu ya kufungashia chupa kwa ajili ya kupelekea sokoni.

**Hatua za usindikaji**

Kabla ya kuanza usindikaji wa togwa, ni muhimu sana kwa msindikaji kuhakikisha kwanza kuwa anafikiria kuhusu soko na mara nyingi soko linaanzia nyumbani kwa watu waliokuzunguka.

**Usindikaji unafanyika kama ifuatavyo;**

Hakikisha unakuwa na mtama na ulezi uliokauka vizuri (ulezi ni kwa ajili ya kutengeneza kimea).

Chambua mtama na ulezi vizuri kwa kutoa uchafu ama taka.

Baada ya kuchambua, safisha kwa kutumia maji safi salama ili kuondoa udongo na vumbi.

Anika juani sehemu safi na salama ili ukauke tena. Saga mtama ili kupata unga. Bandika sufuria jikoni kisha weka maji na ongeza unga tayari kwa kupika uji.

Chemsha mpaka uji uive vizuri (uji usiwe mzito wala mwepesi).

Epua na acha pembeni upoe kisha ongeza kimea (kinachotokana na ulezi). Baada ya saa saba iko tayari kutumika kwa kunywa.

Ili kuhifadhi kwa ajili ya kupeleka sokoni na matumizi ya muda mrefu mara baada ya kuepua acha kwa siku tatu. Rudisha tena jikoni na pasha ili kupata moto kidogo kisha ongeza kilinda chakula (preservative).

Paki ikiwa bado ya moto kwenye chupa maalumu kulingana na ujazo unaopendelewa sokoni. Panga chupa kwenye karatasi maalumu ya kufungashia kisha bana karatasi kwa kuchoma kwa kifaa maalumu ya kuchomea kisha peleka sokoni.

Namna ya kutengeneza kimea

Chukua ulezi mkavu, uoshe na uweke kwenye chombo kikavu alafu ufunike kwa muda wa siku 2. Ukifunua utakuta umeanza kuota (kimea). Chukua ulezi huu kisha saga kidogo ili kubakia na chenga chenga.

Mimina zile chenga chenga za kimea kwenye ule uji na ongeza sukari kidogo.

**Faida za kunywa togwa**

Kinywaji cha togwa kinasadikika kuongeza nguvu, ina madini ya kalsiamu, ina bakteria wazuri wanaohitajika katika mmeng'enyo wa chakula mwilini na kinywaji hiki pia kinaongeza protini mwilini.



# HOWARD HUGHES:
# TAJIRI ALIYEKUFA AKIWA MPWEKE

KUMBUKA jambo moja, hakuna mtu ambaye siwezi kumnunua au kumharibu nikitaka.' Haya ni maneno ya mfanyabiashara tajiri zaidi Marekani wakati huo, Howard Hughes na ulimwengu unamfahamu sio tu kama mfanyabiashara wa viwanda, mtafiti, mtengenezaji wa filamu, shujaa wa zama mpya lakini pia kama mzee wa ajabu, ambaye alitumia miaka 26 ya maisha yake peke yake, akiwa mpweke.

Baadaye mzee huyo alipatwa na wazimu kiasi kwamba aliacha kukata kucha na kuanza kujaza haja ndogo kwenye chupa zake.

**Ilikuwaje?**

Howard Hughes Jr. alizaliwa mwaka wa 1905 na Howard Hughes Sr. Hughes Sr. alikuwa akichimba visima vya mafuta yasiyosafishwa kutoka ardhini na kupata pesa nyingi.

Mkewe, mama wa Howard Hughes Jr., alitoka katika familia ya kifalme. Hughes Sr. alivumbua mashine ya kuchimba visima mwaka wa 1909 ambayo ilibadilisha uso wa uchimbaji mafuta. Walitengeneza visima ambavyo vinaweza kupenya kwenye granite ngumu. Alitengeneza drill kwa jina lake mwenyewe.

Kampuni za mafuta sasa zingepanga mstari kwenye mlango wa Hughes Sr. na kusubiri mashine ya kuchimba visima ifike. Hughes Sr. alipata pesa nyingi.

Mama Howard naye alikuwa akihangaikia sana usafi. Lazima niseme kichaa. Tabia hiyo hiyo baadaye ilishuka kwa Howard. Howard alikuwa dhaifu na mgonjwa wakati wa kuzaliwa. Hakuweza kusikia kwa sikio moja. Mama Howard alimtunza sana kwa sababu hii.

Kwa hivyo labda baba yake kila wakati alimpeleka shule tofauti za bweni. Hakuna wasiwasi juu ya kuingia huko, kwa sababu kitabu cha hundi cha baba ya Howard kilikuwa tayari kila wakati.

Howard alikuwa mvulana mwenye haya, kiziwi kidogo. Hangeathiriwa na jinsi watu wawili wakubwa wa nyumba hiyo walivyomtendea.

Hakutaka kuongea na mtu yeyote shuleni. Hatimaye alipata njia mbili za kuondokana na upweke wake - sinema na ndege.

Alikuwa na shauku ya uvumbuzi. Alipokuwa na umri wa miaka kumi na minne, baba yake alimpeleka kwenye mashindano ya kupiga mbizi kati ya vyuo vikuu viwili vya Marekani.

Baba akamwambia ukishiriki shindano hilo na kushinda nitakupa zawadi uliyoomba. Howard alishinda shindano hilo na akamwomba baba yake dola tano.

Kwa sababu pale mashindano yalipokuwa yakifanyika, kulikuwa na tangazo la ndege ya chini kabisa, na Howard alitaka kupanda ndege. Alikuwa ametoka kushinda mbio za kupanda ndege hiyo.

Mama ya Howard alifariki miaka miwili baadaye, na baba yake miaka miwili baadaye. Howard mwenye umri wa miaka 18, ambaye hata hakumaliza elimu yake, alipata utajiri wote.


Howard alikuwa na hakika kwamba hakuna kitu ambacho angeweza kufanya kwa pesa za baba yake. Ingawa baba yake alikuwa katika biashara ya kuchimba mafuta, Howard hakupendezwa. Alijitosa Hollywood.

**Tabia ya ajabu**

Baada ya kuingia Hollywood, Howard alianza kufuja pesa za baba yake. Tabia ya Howard Hughes imeandikwa na Peter Henry Brown na Pat Brosek. Anaandika katika kitabu chake, "Hughes hakuwahi kununua jozi ya viatu vya gharama kubwa, alinunua jozi 20. Hakuwahi kununua gari, alinunua magari 6."

"Alikuwa akinunua masanduku ya saa za bei ghali sana. Aliwahi kununua suti 20 mara moja."

Ilikuwa wakati huo ambapo aliwafukuza jamaa zake kutoka kwa kampuni ya baba yake. Alinunua hisa kwa dola milioni 3.8. Alikuwa anaenda kumwaga pesa zote za kampuni ya baba yake kwenye jumba la sinema.



**Itaendelea kesho**



# SAUDIA



## MACHO KWA VINCIUS Jr

RIYADH, Saudia

**KLABU za Saudi Arabia bado vina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Real Madrid Vinicius Jr, 24, nchini humo - huku mtendaji mkuu wa ligi hiyo akisema kuhama ni "suala la muda".**

Nayo Chelsea wanataka pauni milioni 40 kumuachilia beki Muingereza Trevoh Chalobah baada ya kumrejesha mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 25 kutoka Crystal Palace.

Mchezaji mwingine wa Chelsea, Cesare Casadei mwenye umri wa miaka 22, huenda akaelekea Lazio baada ya vilabu hivyo viwili kukaribia kuafikiana.


## ARSENAL, FOREST VITA KWA CUNHA


LONDON, England

**MABOSI wa Nottingham Forest wanataka kumsajili Matheus Cunha Januari hii, Arsenal pia wameonyesha nia ya kutaka kumsaini mshambuliaji huyo wa Wolves.**

Nottingham Forest kwa sasa inamtaka kwa udi na uvumba mshambuliaji huyo wa Wolves na Brazil, Matheus Cunha kuwa shabaha yao kuu ya Januari katika harakati za kufuzu Ligi ya Mabingwa.

Arsenal pia wameonyesha nia ya kutaka kumsajili Cunha mwenye umri wa miaka 25 katika uhamisho wa Januari.





## CHELSEA BADO KWA GARNACHO

LONDON, England

**TIMU ya Chelsea wanatazamiwa kufanya mazungumzo zaidi na Manchester United kuhusu winga wa Argentina Alejandro Garnacho, 20, ambaye thamani yake ni pauni milioni 50.**

Wakati hayo yakiendelea, Manchester United imewaulizia wachezaji wa Bournemouth na Hungary Milos Kerkez, 21, Wolves na Algeria Rayan Ait-Nouri, 23, na kiungo wa Crystal Palace na Muingereza Tyrick Mitchell, 25, huku kipaumbele cha Ruben Amorim kikiwa kumsajili winga wa kushoto.

## CITY IPO KWA LUIZ

MANCHESTER, England

**TIMU ya Manchester City wanataka kumsajili kiungo wa Brazil Douglas Luiz kutoka Juventus, Ligi ya Saudi Arabia bado inamnyatia Vinicius Jr, Chelsea kumuachia Trevoh Chalobah wakipata £40m.**


Manchester City pia wanafikiria kumsajili kwa mkopo kiungo wa Brazil Douglas Luiz, 26, ingawa Juventus inashinikiza wajibu wa kumsaini ili kujumuishwa katika mpango huo uliopendekezwa.



Mjasiriamali spoti

MJASIRIAMALI JANUARI 23, 2025

Tovuti: www.mjasiriamali.co.tz



# YANGA NGUVU LIGI KUU

NA ASHA SEKEFU

**YANGA imesema, kwa sasa hasira zake zote zinarejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kuondoshwa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambapo walifika hatua ya makundi.**

Kutokana na kuondolewa huko, Yanga imesema ina maumivu makubwa kwani pamoja na kutimiza lengo lao la kufika makundi katika hatua hiyo, lakini kutolewa huku wakiwa na nafasi ya kusonga mbele imewaumiza mno.

Meneja Habari na Mawasiliano Yanga, Ali Kamwe amekiri maumivu ya kutolewa kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwao ni darasa tosha na sehemu ya wamejifunza nini cha kufanya, ili wasije kuumia zaidi mbele ya safari.

Kamwe amesema maumivu wanayopata kwa kuondolewa kwenye makundi wanaweza kuhisi makubwa na mazito, wanatakiwa kutumia nafasi hii kujiuliza na kujipanga kwa ajili ya kutetea mataji ya Ligi Kuu na Kombe la Shirikisho la FA.

"Tukipoteza makombe yetu tuliyopata msimu uliopita, maumivu haya yatakuwa maumivu makali mara mbili au zaidi. maumivu haya yawe darasa na sehemu ya kupambana kufanya vizuri, tusije kuumia zaidi, tumegundua furaha yetu inawaumiza wapinzani wetu, basi tushikamane," alisema.

Kamwe alisema, sasa nguvu na akili zao wanatakiwa kuelekeza katika michuano iliyopo mbele yao ya Ligi Kuu na michuano ya kombe la FA kuhakikisha wanafanikiwa kutetea mataji hayo.

"Tunahitaji kufanya vizuri katika michezo yetu ya ligi kukusanya alama tatu kila mechi na kurejea kwenye nafasi yetu ya kuongoza ligi na kufanya vizuri michuano ya FA," alisema Kamwe.

Yanga inatarajiwa kushuka dimba la KMC Complex, kwenye mchezo wa michuano ya Kombe la Shirikisho la FA dhidi ya Copco FC, utakaochezwa, Jumamosi, Januari 25.

## STAA SIMBA WATOA NENO

NA MIMI-NEEMA CHARLES

**WACHEZAJI Simba wametoa yao ya moyoni na kusema, kufanikiwa kutinga robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, huku wakiongoza kundi lao kumeifanya timu hiyo izidi kuogopwa zaidi barani Afrika.**

Akizungumza kwa niaba yao, Nahodha wa Simba, Mohammed Hussein `Zimbwe Jr, amesema kumaliza kinara wa kundi kwenye michuano kombe la Shirikisho Afrika kumewapa nafasi ya kumewafanya wazidi kuwa tishio barani Afrika.

Simba hatua inayofuata ya robo fainali inatarajiwa kucheza na kati ya Stellenbosch ya Afika Kusini, Al Masry ya Misri au Asec Mimosa ya Ivory Coast.

"Kwa `Level`ya Simba ilipofikia sio kuogopa timu au mpinzani yoyote anayekuja mbele yetu, siku zote unapomaliza nafasi ya juu unatengeneza nafasi ya mpinzani kukuogopa," amesema.

Zimbwe Jr amesema baada ya kufanikiwa sasa wanahitaji kuona Simba inaendelea kufanya vizuri katika hatua inayofuata na kucheza nusu fainali.

"Simba bado haijawa imara kama ilivyokuwa misimu mitatu au minne, lakini taratibu tunarudi kwenye ubora wetu kwa kuwa tishio kwa mashindano ya ndani na nje," amesema.

